**Uambatanishaji katika Lugha ya Kiswahili**

JLLE
Vol 19(1) 53–66
© The Publisher
DOI:10.56279/jlle.v19i1.5

*Luinasia Elikunda Kombe*[1]

**Ikisiri**
*Makala hii inahusu uambatanishaji katika lugha ya Kiswahili. Lengo ni kuonesha upekee wa lugha ya Kiswahili katika uambatanishaji ili kubaini ufanano na utofauti uliopo baina ya lugha ya Kiswahili na lugha nyingine. Miongoni mwa mambo yaliyojadiliwa katika makala hii kuonesha upekee huo ni aina za uambatanishaji katika lugha ya Kiswahili, aina za viunganishi ambatanishi, idadi na mtawanyo wa viunganishi ambatanishi katika tungo ambatani na namna viunganishi ambatanishi vinavyotofautiana kulingana na aina na idadi ya viambatanishwa. Data za makala hii ni za utafiti wangu wa uzamivu zilizokusanywa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa matini. Uchanganuzi wa data hizo katika makala hii umeongozwa na Nadharia Msingi ya Isimu. Matokeo yanabainisha kuwa, Kiswahili kina aina mbili za uambatanishaji, yaani uambatanishaji kwa kiunganishi dhahiri na uambatanishaji bila kiunganishi dhahiri. Pia, imebainika kuwa lugha ya Kiswahili ina aina mbalimbali za viunganishi ambatanishi na ni lugha inayotumia kiunganishi kimoja katika kuunganisha viambatanishwa viwili. Halikadhalika, imebainika kwamba viunganishi ambatanishi vya Kiswahili hutofautiana kimatumizi kwani vipo vinavyoambatanisha virai na vishazi na vinavyoambatanisha vishazi pekee. Pia, imebainika kwamba kuna vinavyoambatanisha viambatanishwa viwili tu na vinavyoambatanisha viambatanishwa zaidi ya viwili*.

**Maneno msingi**: *Uambatanishaji, viambatanishwa, viunganishi ambatanishi, tungo ambatani*

**Abstract**
***This article focuses on coordination in the Kiswahili language.*** *The aim is to demonstrate the uniqueness of Kiswahili in coordination in order to identify the similarities and differences between Kiswahili and other languages. Among the aspects discussed to highlight this uniqueness are: the types of coordination in Kiswahili, types of coordinating conjunctions, distribution of coordinating conjunctions in coordination constructions, and how coordinating conjunctions vary based on the type and number of conjuncts. Data presented in this article are drawn from my doctoral research, collected through textual analysis methods. Data analysis in this article was carried out using a qualitative approach by the guidance of Basic Linguistic Theory. The findings reveal that Kiswahili exhibits two types of coordination: coordination with an overt conjunction and coordination without an overt conjunction. It is also found that Kiswahili has a variety of coordinating conjunctions and typically uses a single conjunction to link two coordinated elements. Furthermore, the study reveals that Kiswahili coordinating conjunctions differ in usage; some are used to coordinate both phrases and clauses, while others coordinate clauses only. Additionally, some conjunctions coordinate only two conjuncts, whereas others can coordinate more than two conjuncts*.

**Keywords:** *Coordination, conjuncts, coordinating conjunctions, coordinate constructions*

**Utangulizi**[2]

Tafiti zinaonesha kwamba lugha nyingi ulimwenguni zinaonekana kuwa na tungo ambatani za aina fulani, ingawa kuna tofauti nyingi za kiisimu baina ya lugha moja na nyingine (Camacho, 2003; Haspelmath, 2004; Drellishak, 2004; Zhang, 2009). Tofauti hizo zimetokana na lugha kuwa na namna mbalimbali za uambatanishaji zenye mahitaji tofauti kisintaksia na ambazo hutofautiana kati ya lugha na lugha (Haspelmath, 2004). Kwa mfano, tafiti zinaonesha kuwa kuna lugha zenye viunganishi ambatanishi dhahiri kimofolojia na nyingine zina viunganishi

[1] **Corresponding author:**
Luinasia Elikunda Kombe, Department of Languages and Literature, Dar es Salaam University College of Education, University of Dar es Salaam, Dar es Salaam, Tanzania. E-mail: kombeluinasia@gmail.com

[2] Makala hii ni zao la tasinifu yangu ya uzamivu inayohusu uchambuzi wa sintaksia ya uambatanishaji katika lugha ya Kiswahili. Data za utafiti zilipatikana katika machapisho mbalimbali ya kifasihi, magazeti, hotuba na ripoti za serikali.

visodhahiri, yaani visivyodhihirishwa kimofolojia. Pia, baadhi ya lugha zina maumbo mawili au zaidi ya kiunganishi kimoja ambayo hutumika kulingana na kategoria ya viambatanishwa. Tofauti hizo zimetokana na lugha kuwa na namna mbalimbali za uambatanishaji zenye mahitaji tofauti kisintaksia yanayotofautiana kati ya lugha moja na nyingine. Kutokana na tofauti hizo, Haspelmath (2004) anaeleza kuwa baadhi ya lugha zina utajiri mkubwa wa tungo ambatani zinazohusiana kwa namna changamani sana. Hivyo, ni wazi kuwa suala la uambatanishaji ni suala la lugha mahususi. Kutokana na umahususi huo, makala hii inalenga kushughulikia uambatanishaji katika lugha ya Kiswahili ili kuonyesha namna Kiswahili kinavyofanana na kutofautiana na lugha nyingine katika mchakato wa uambatanishaji.

Haspelmath (2004, 2007) anaeleza kwamba uambatanishaji ni mchakato wa kisintaksia wa kuweka pamoja vipashio viwili au zaidi vya aina moja ili kuunda kipashio kikubwa zaidi, bila kupoteza mahusiano ya asili ya kisemantiki na elementi nyingine za karibu. Hii ina maana kuwa tungo yenye sehemu mbili (tuseme A na B) itatambuliwa kuwa ni tungo ambatani ikiwa sehemu hizo mbili zitakuwa na hadhi sawa. Hivyo, tungo ya kingazi au kidarajia ambayo sehemu yake mojawapo inachomoza au ni ya muhimu zaidi, wakati sehemu nyingine kwa namna fulani ni tegemezi haiwezi kuwa tungo ambatani.

Kutokana na maelezo haya, ni wazi kuwa ili kupata tungo ambatani inayokubalika kisarufi, sharti vipashio vinavyoambatanishwa viwe vya kategoria moja au vyenye hadhi sawa kama mfano namba (1) unavyoonesha.

1. [Wapo walioacha kabisa uzalishaji] na [wengine waliofunga hata mitambo ya uzalishaji]. (Magufuli 20/11/2015:10)

Vipashio vilivyoambatanishwa katika mfano namba (1) vimewekwa kwenye mabano mraba. Vipashio hivyo ni vya kategoria moja, yaani vishazi tegemezi. Vipashio hivyo vimeambatanishwa kwa kiunganishi ambatanishi ‘na’.

Miongoni mwa mambo yanayotofautisha lugha moja na nyingine kiuambatanishaji ni pamoja na aina za uambatanishaji, aina na idadi ya viunganishi ambatanishi kisemantiki na kimofolojia, mtawanyo wa viunganishi ambatanishi katika tungo ambatani na matumizi ya viunganishi ambatanishi kulingana na aina na idadi ya viambatanishwa[3] (taz. Haspelmath, 2004). Hivyo, makala hii inalenga kutumia vipengele hivyo kubainisha ufanano na utofauti uliopo baina ya lugha ya Kiswahili na lugha nyingine katika suala la uambatanishaji.

**Methodolojia**

Data zilizotumika katika makala hii ni za upili kwa kuwa ni data zilizotumika katika utafiti wa uzamivu wa (Kombe, 2019). Data hizo alizipata kwa njia ya uchambuzi wa matini mbalimbali zikiwemo za kisiasa, kifasihi na magazeti. Kulingana na malengo na nadharia iliyotumika katika makala hii, data hizo zimechanganuliwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli. Uchambuzi wa data umefanyika kwa mbinu ya uchambuzi wa kidhamira kwa kuongozwa na misingi ya Nadharia Msingi ya Isimu. Baada ya sehemu hii ya methodolojia, sehemu inayofuata inahusu nadharia iliyotumika katika makala hii ambayo ni Nadharia Msingi ya Isimu.

**Nadharia Msingi ya Isimu**

Makala hii imetumia Nadharia Msingi ya Isimu ya Dixon (2010) kufafanua uambatanishaji katika lugha ya Kiswahili. Katika nadharia hii Dixon anasisitiza kuwa Nadharia Msingi ya Isimu inapaswa kufafanua kila lugha kwa misingi yake yenyewe kuliko kufafanua lugha fulani mahususi kwa kutumia misingi ya lugha nyingine. Dryer (2001) anaielezea nadharia hii kama mkabala wa kinadharia unaotumiwa sana katika ufafanuzi wa lugha hasa sarufi ya lugha. Inaeleza kuwa ni nadharia yenye mkusanyiko wa mawazo kutoka katika mikabala mingi kuanzia Sarufi Mapokeo, Sarufi Miundo Virai, Sarufi Zalishi na Sarufi Uhusiano. Kwa ujumla, hii ni nadharia iliyokua taratibu kadiri wanaisimu walivyozidi kujifunza namna bora ya kufanya ufafanuzi wa lugha.

Nadharia Msingi ya Isimu inatoa mbinu na taratibu maalum za kueleza masuala ya kiisimu kwa kutumia kanuni majumui na ruwaza za kitaipolojia baina ya lugha. Kwa maneno mengine, nadharia hii inasisitiza kueleza na kufafanua vipengele vya lugha kwa utaratibu maalumu, sambamba na kulinganisha lugha ili kubaini tabia majumui na tabia mahususi za lugha, yaani kufanana na kutofautiana kwa lugha. Pia, inasisitiza umuhimu wa usahihi wa ufafanuzi na utaratibu wa uchambuzi wa data. Inataka masuala ya kisarufi ya lugha fulani mahususi yaelezwe vile yalivyo kwa usahihi na kwa utoshelevu bila kutumia modeli za lugha nyingine kuyaelezea.

Nadharia Msingi ya Isimu ina misingi mitano. Msingi wa kwanza ni umajumui wa lugha. Kupitia msingi huu, Nadharia Msingi ya Isimu inaamini kwamba pamoja na wingi wa lugha ulimwenguni, kuna ruwaza, kanuni,

---

[3] Viambatanishwa ni vipashio vinavyounganishwa kwa viunganishi ambatanishi. Kiingereza vinaitwa *conjuncts*.

kategoria na miundo ambayo ni majumui. Msingi huu unataka masuala majumui yabainishwe na kufasiliwa kwa lengo la kuona tabia majumui katika mfumo wa lugha na kuboresha uainishaji wa taipolojia za lugha. Msingi wa pili ni ulinganishaji wa kitaipolojia. Msingi huu unataka maarifa ya kitaipolojia yatumike katika uchunguzi wa kiisimu ili kubaini ufanano na utofauti uliopo baina ya lugha. Msingi wa tatu ni uchambuzi wa kidhima. Katika msingi huu Nadharia Msingi ya Isimu inasisitiza uelewa wa masuala ya kiisimu kama vile miundo ya kiisimu kulingana na dhima zake katika lugha. Hii ni pamoja na kuchunguza namna elementi za kisarufi zinavyotimiza lengo la mawasiliano na kuchangia maana. Msingi wa nne ni usahihi wa kiuelezi. Katika msingi huu, nadharia inasisitiza usahihi na ufafanuzi wa kina wa data za kiisimu. Msingi huu unataka ufafanuzi wa data ufanyike kwa kina ili jambo linalochunguzwa liweze kuelezwa kwa kina na kwa usahihi. Msingi wa tano ni utaratibu maalumu wa uchambuzi wa data. Nadharia Msingi ya Isimu inataka kuwe na utaratibu maalumu katika uchambuzi wa data za kiisimu. Hii ni pamoja na kuzingatia urari wa methodolojia na kanuni katika kuchunguza vipengele mbalimbali vya lugha katika ngazi zote kuanzia fonolojia, mofolojia, semantiki hadi sintaksia.

Misingi yote imetumika katika makala hii kueleza namna uambatanishaji unavyofanyika katika lugha ya Kiswahili. Msingi wa kwanza umetumika kuonesha vipengele majumui vya uambatanishaji vilivyopo katika lugha ya Kiswahili. Msingi wa pili umetumika kuonesha namna vipengele vyote vya uambatanishaji vilivyojadiliwa katika makala hii vinavyofanana na kutofautiana na lugha nyingine. Msingi wa tatu ambao ni uchambuzi wa kidhima umetumika kuonesha namna viunganishi ambatanishi vya Kiswahili vinavyotumika kulingana na aina na idadi ya viambatanishwa kwa kutoa dhima za viunganishi hivyo katika muundo na maana ya tungo. Msingi wa nne ambao ni usahihi wa kiuelezi umetumika kutoa ufafanuzi sahihi wa kina juu ya uambatanishaji katika lugha ya Kiswahili. Ufafanuzi huo umefanyika baada ya uchambuzi wa kina wa data za utafiti. Msingi wa tano ambao unahusu utaratibu maalumu wa uchambuzi wa data umetumika katika uchambuzi wa data za utafiti huu. Kwa kutumia msingi huu, uchambuzi wa data umefanyika kwa kutumia mkabala wa kitaamuli na mbinu ya uchambuzi wa kimaudhui. Sehemu inayofuata inahusu mjadala juu ya vipengele vya uambatanishaji vilivyolengwa katika makala hii ili kuonesha ufanano na utofauti uliopo baina ya lugha ya Kiswahili na lugha nyingine.

**Aina za Uambatanishaji katika Lugha ya Kiswahili**

Tafiti zinaonesha kuwa kuna aina mbili za uambatanishaji (Haspelmath, 2000; 2004). Kuna uambatanishaji kwa kutumia viunganishi ambatanishi dhahiri kimofolojia na bila viunganishi dhahiri, yaani visivyodhihirika kimofolojia. Viunganishi dhahiri kimofolojia vinaweza kuwa maneno, viambishi au viangami na viunganishi visodhahiri ni kiimbo kinachowakilishwa kwa alama ya mkato (Haspelmath, 2004). Kwa mujibu wa Nadharia Msingi ya Isimu, aina hizi za uambatishaji ni kipengele majumui katika uambatanishaji. Data zinaonyesha kwamba lugha ya Kiswahili ni miongoni mwa lugha zenye aina zote mbili za uambatanishaji, yaani uambatanisaji wa kutumia viunganishi dhahiri kimofolojia na ule wa bila viunganishi dhahiri.

Uambatanishaji wa bila kiunganishi dhahiri hufanyika kwa njia ya kiimbo cha uambatanishaji. Katika lugha ya maandishi, kiimbo cha uambatanishaji huwakilishwa kwa alama ya mkato. Data zinaonesha kuwa matumizi ya alama ya mkato inayowakilisha kiimbo cha uambatanishaji katika lugha ya Kiswahili huweza kutumika peke yake bila kiunganishi dhahiri kuambatanisha vipashio vya lugha ya Kiswahili. Namna ya pili, alama ya mkato hutumika sambamba na kiunganishi dhahiri. Hali hii imeelezwa pia na Mithun (1988) kwamba katika baadhi ya lugha kiimbo huweza kutumika bila kiunganishi dhahiri kuambatanisha vipashio na huweza kuambatana na kiunganishi dhahiri. Alama ya mkato inayowakilisha kiimbo inapotumika sambamba na kiunganishi huwa na dhima ya kutenga viambatanishwa vilivyobeba dhana tofauti. Tazama mifano namba (2a na b) kwa ufafanuzi.

2. (a) [[Alirusha mkono wake kama mtu aliyeumwa na nge], na [alipotazama kidole chake aliona kinatoka damu]]. (Abdulla, 1997:18)

   (b) [[Amenyosha miguu upande wa kibla], na [kumuashiria mama yake aje kumfunika tena. (Abdulla, 1997:23)

Tungo ambatani katika mifano (2a na b) zina viambatanishwa viwili vilivyoko kwenye mabano na vimeambatanishwa kwa kiunganishi *na*. Alama ya mkato imetumika sambamba na kiunganishi ambatanishi kwa lengo la kuvitenga viambatanishwa kwa sababu vimebeba dhana tofauti. Hii ina maana kwamba, ikiwa viambatanishwa vimebeba dhana zinazohusiana, alama ya mkato inayowakilisha kiimbo huwa haitumiki sambamba na kiunganishi dhahiri kwani dhana hizo hazitakiwi kutengwa. Hivyo, alama ya mkato ikiambatana na kiunganishi dhahiri hutumika kuonesha kwamba dhana zilizobebwa na kila kiambatanishwa hazihusiani.

Alama ya mkato inayowakilisha kiimbo cha uambatanishaji inapotumika peke yake bila kiunganishi dhahiri huwa na dhima ya kuambatanisha vipashio. Alama hiyo huwekwa baada ya kiambatanishwa cha kwanza katika tungo

ambatani yenye viambatanishwa viwili. Pia, huwekwa baada ya kila kiambatanishwa, isipokuwa katika kiambatanishwa cha mwisho katika tungo yenye viambatanishwa vingi. Mifano ya (3a na b) inaonesha alama ya mkato ya kiimbo cha uambatanishaji inavyotumika kuambatanisha vipashio katika lugha ya Kiswahili.

3. (a) [[Huyu anapika mkate wa mtabaka], [yule kuku wa kupaka]]. (Mohamed, 2007:38)

   (b) [[Wale wageni wote walianza kucheka cheka], [wenyeji nao ikabidi wacheke bila kujua hasa wenzao wanacheka nini]]. (Mohamed, 2007:42)

Viambatanishwa vilivyoko kwenye mabano mraba katika mifano ya (3a na b) vimeambatanishwa bila kiunganishi dhahiri. Alama ya mkato inayowakilisha kiimbo cha uambatanishaji ndiyo iliyotumika kama kiunganishi ambatanishi. Alama hiyo imewekwa baada ya kiambatanishwa cha kwanza. Alama hiyo imetumika peke yake kuambatanisha vipashio hivyo bila kiunganishi dhahiri.

Mithun (1988) anaeleza kwamba kiimbo ni njia ya asili ya uambatanishaji kwa sababu tafiti zinaonesha kwamba, kabla ya mfumo wa maandishi lugha zilitumia kiimbo kuambatanisha vipashio mbalimbali. Hoja hii inaungwa mkono na Haspelmath (2004:7) kwamba lugha zilizochelewa kupata mfumo au utamaduni wa maandishi hutumia zaidi kiimbo kuambatanisha vipashio kuliko viunganishi ambatanishi dhahiri. Kwa hiyo, kadri mfumo wa maandishi unavyozidi kuimarika, lugha hutafuta leksika zitakazotumika kama viunganishi dhahiri katika maandishi. Hata hivyo, Mithun (keshatajwa) anaeleza kwamba tafiti zinaonesha kuwa lugha nyingi duniani hutumia kiimbo hata baada ya kupata viunganishi ambatanishi dhahiri. Utafiti huu unaonesha kuwa Kiswahili ni miongoni mwa lugha hizo ambazo hutumia kiimbo hata baada ya kupata viunganishi ambatanishi dhahiri. Pamoja na matumizi hayo ya kiimbo, data zinaonesha kuwa umbatanishaji katika lugha ya Kiswahili hufanyika zaidi kwa viunganishi dhahiri. Kwa mujibu wa Nadharia Msingi wa Isimu, data na ufafanuzi wake katika kipengele hiki unadhihirisha upekee wa lugha ya Kiswahili.

**Uambatanishaji kwa Kutumia Viunganishi Dhahiri katika Lugha ya Kiswahili**

Tafiti zinaonesha kuwa uambatanishaji kwa kutumia viunganishi dhahiri ni ule unaotumia kiunganishi ambacho ni neno, kiambiashi au kiangami vinavyodhihirika kimofolojia na kifonolojia kuambatanisha vipashio (Haspelmath, 2004). Katika lugha ya Kiswahili, viunganishi ambatanishi dhahiri ni maneno huru. Mifano namba (4a–c) inafafanua zaidi.

4. (a) [[Sehemu kubwa maafa] **na** [sehemu ndogo nafuu]]. (Mohamed, 2007:5)
   (b) [[Ukizitazama utaona upuuzi], **lakini** [ukizingatia utaona ni ukweli]. (Abdulla,1997:23)
   (c) [[Tafiti zinasaidia kuwepo] **au** [kudumu kwa watu na dola]]. (Mwananchi 29/6/2017:4)

Viambatanishwa katika mifano (4a–c) vimeunganishwa kwa viunganishi dhahiri ambavyo ni maneno. Viunganishi hivyo vimeandikwa kwa wino uliokozwa. Tofauti lugha zinazotumia viambishi na viangami kuambatanisha vipashio, Kiswahili hutumia maneno.

**Aina za Viunganishi Ambatanishi Ambavyo ni Maneno Huru**

Kiswahili kina utajiri mkubwa wa viunganishi ambatanishi ambavyo ni maneno huru ingawa kwa asilimia kubwa viunganishi hivyo vimekopwa kutoka lugha ya Kiarabu (Ashton, 1947). Katika utafiti huu, viunganishi hivyo vimewekwa katika makundi manne kulingana na semantiki ya kila kiunganishi husika. Makundi hayo ni viunganishi viongezi, viunganishi vichaguzi, viunganishi tenguzi, viunganishi kanushi na viunganishi vya wakati.

*Viunganishi Ambatanishi Viongezi*

Hivi ni viunganishi ambavyo huambatanisha vipashio kiuongezi; yaani maana ya kiambatanishwa cha pili huongezwa katika ile maana ya kiambatanishwa cha kwanza na kuunda maana mbili za aina moja. Viunganishi viongezi vilivyobainishwa katika utafiti huu ni “na”, “pamoja na”, “tena” na “pia”. Mifano ya (5a–e) inaonesha namna viunganishi hivi vinavyotumika kuunda tungo ambatani.

5. (a) ...kuhakikisha migogoro ya ardhi [[tunaitatua] **na** [kuikomesha]]. (Magufuli 20/11/2015:21)

   (b) Aliona kitu [[kisafi kabisa] **tena** [chekundu]]. (Abdulla, 1997:12)

(c) Kudhibiti [[biashara ya fedha haramu], **pamoja na** [ufadhili wa ugaidi]]. (Wizara ya Fedha 2016/2017:6)
(d) [[...kuimarisha mipango ya usalama mahali pa kazi], **pia** [kufanya ukaguzi wa mara kwa mara]]. (Mtanzania 30/4/2017:3)

Viunganishi ambatani vilivyotumika katika mifano ya (5a-d) ni viunganishi viongezi kwa sababu vimeweka pamoja kiuongezi maana ya vipashio vya lugha vilivyoko kwenye mabano. Mfano wa (5a) unaonesha tendo la "kuitatua migogoro" na tendo la "kuikomesha" yamewekwa pamoja kiuongezi na kuwa matendo mawili yatakayofanywa pamoja. Vivyo hivyo, katika mfano (5b), virai vivumishi "kisafi kabisa" na "chekundu" vimeambatanishwa kiuongezi kwa kiunganishi "tena" na kuwa sifa mbili za kitu kilichoonwa.

Vilevile, katika mfano wa (5c) virai nomino "biashara ya fedha haramu" na "ufadhili wa ugaidi" vimeunganishwa kiuongezi kwa kiunganishi "pamoja na" na kuunda virai nomino viwili vinavyojaliza kitenzi "kudhibiti". Kifungu cha maneno 'pamoja na' kinatumika kama kiunganishi kimoja kuunganisha vipashio. Halikadhalika, katika mfano wa (5d), kiunganishi "pia" kimeambatanisha kiuongezi vishazi visoukomo "kuimarisha mipango ya usalama mahali pa kazi" na "kufanya ukaguzi wa mara kwa mara" kuwa vishazi viwili vinavyoelezea matukio mawili yanayotakiwa kufanyika kwa pamoja. Kwa mujibu wa tafiti zilizotangulia, lugha nyingi ulimwenguni zina viunganishi viongezi ila idadi ya viunganishi hivyo na nafasi yake katika tungo huweza kutofautiana kati ya lugha na lugha (taz. Haspelmath, 2004; Drellishak, 2005; Zhang, 2009). Katika utafiti huu, viunganishi viongezi vilivyobainishwa katika lugha ya Kiswahili ni vinne na huwekwa katikati ya viambatanishwa viwili kama mifano (5a-d) inavyoonesha.

Tafiti zinaonesha kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya viunganishi ambatanishi viongezi na vielezi kwani kihistoria inadaiwa kuwa chanzo au asili ya viunganishi hivyo katika lugha nyingi ulimwenguni ni vielezi (Mithun, 1988: 244-249; Ramat na Mauri, 2011:3). Kwa mfano, Mithun (1988) anaeleza kuwa, katika lugha ya Kiingereza, chanzo au asili ya kiunganishi *and "*na" ni kihusishi *with* "na" pamoja na vielezi vingine kama *also* "pia" na *then* "kisha". Hili linadhihirika katika lugha ya Kiswahili kinganishi ongezi neno "na" hutumika pia kama kihusishi. Pia, viunganishi viongezi "pia" "tena" na neno 'pamoja' navyo hutumiwa kama vielezi katika lugha ya Kiswahili. Tazama mifano (6a-d).

6. (a) Wageni walikuja **na** zawadi
   (b) Dada alikuja **pamoja na** rafiki zake
   (c) Wanafunzi waliimba **pia**
   (d) Watoto hawaumwi **tena**
   (Chanzo: Mtafiti 2024)

Neno "na" katika mifano (6a na b) ni kihusishi na maneno "pamoja", "pia" na "tena" katika mifani (67b-d) ni vielezi. Maana inayopatikana na nafasi za maneno hayo katika tungo hizo inathibitisha kuwa maneno hayo katika tungo hizo sio viunganishi ambatanishi. Hii inathibitisha kwamba hata katika lugha ya Kiswahili, kiunganishi 'na' kimetokana na kihusishi "na". Tofauti kati ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza ni kwamba Kiswahili kinatumia "na" kama kiunganishi na kihusishi wakati Kiingereza kina maumbo mawili tofauti kwa ajili ya kihusishi na kiunganishi. Aidha, data zinathibitisha kuwa, maneno mengine yanayotumika kama viunganishi ambatanishi viongezi ni vielezi. Hii ina maana kwamba kama ilivyo katika lugha nyingine Kiswahili hutumia maumbo ya vielezi kama viunganishi ambatanishi. Hivyo, Kiswahili kinathibishisha kilichoelezwa na (Mithun (1988: 244-249) na Ramat na Mauri (2011:3) kwamba chanzo cha viunganishi ambatanishi viongezi katika lugha nyingi ulimwenguni ni vihusishi na vielezi.

*Viunganishi Ambatanishi Vichaguzi*

Viunganishi vichaguzi vilivyobainishwa katika utafiti huu ni "au" na "ama". Viunganishi hivi huitwa viunganishi vichaguzi kwa sababu kisemantiki viunganishi hivi hutenga viambatanishwa kwa kutoa fursa ya kuchagua jambo moja kati ya mambo mawili yaliyoambatanishwa. Mifano ya (7a na b) inafafanua zaidi namna viunganishi hivi vinavyotumika kuunda tungo ambatani za Kiswahili.

7. (a) Mawakala walipewa fursa ya kueleza [kuridhika] **au** [kutoridhika]] kwao na mwenendo wa upigaji kura. (Tume ya Taifa ya Uchaguzi Mkuu, 2015:49)
   (b) Mashirika ya kimataifa [kwa namna moja] **ama** [nyingine]] yamesaidia katika utekelezaji wa bajeti ya wizara. (Wizara ya Fedha, 2016/2017:6)

Katika mifano ya (7a na b), viambatanishwa vilivyoko kwenye mabano vimeambatanishwa kiuchaguzi na si kiuongezi. Mathews (2007) anaeleza kuwa huu ni uambatanishaji unaotenganisha vibadala. Kwa mfano, katika (7a), "kuridhika" na "kutoridhika" ni vibadala ambavyo vyote vinakidhi sifa ya "kuelezwa". Hivyo, kiunganishi 'au" kinaashiria hali ya uchaguzi kati ya vibadala hivyo. Kuchagua kati ya vibadala hivyo maana yake ni kuvitenga na si kuviweka pamoja. Vilevile, katika mfano wa (7b), uchaguzi unaoashiriwa na kiunganishi "ama" unavitenga vibadala "namna moja" na "namna nyingine".

Katika mifano namba (7a na b) tumeona kuwa maumbo "au" na "ama" ni viunganishi ambatanishi katika lugha ya Kiswahili. Kwa mujibu wa data ya utafiti huu, kuna tungo ambatani ambazo zimetumia kiunganishi "au" na "ama" kwa pamoja. Aidha, wataalamu mbalimbali kama Dik (1968: 34-37) na Oirsow (1987:106) wanaeleza kwamba kwa kawaida katika lugha za kiunganishi kimoja, viunganishi ambatanishi hupishana kimtoano, yaani vipashio viwili haviwezi kuambatanishwa kwa zaidi ya kiunganishi ambatanishi kimoja. Hii ina maana kwamba tungo ambatani zilizobainishwa katika utafiti huu zenye viunganishi "ama…au…" ni tungo ambatani ambazo viambatanishwa vyake vimeambatanishwa kwa kiunganishi kimoja na si vyote viwili. Tuchunguze mifano ya (a na b) kwa ufafanuzi zaidi.

8. (a) Mtu aliyewahi kutiwa hatiani kwa ubadhirifu wa mali ya umma, [[**ama** katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano] **au** [Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar]] hatakuwa na sifa ya kuteuliwa. (Katiba Inayopendekezwa 2004:39)
   (b) Haitaruhusiwa kufungua shauri la madai kuhusu jambo lolote alilolitenda rais [[**ama** kabla] **au** [baada ya kushika madaraka]]. (Katiba Inayopendekezwa 2004:32)

Mifano ya (8a na b) inadhihirisha kuwa kiunganishi ambatanishi katika tungo hizo ni "au" na si "ama". Neno "ama" katika tungo hizo halifanyi kazi ya kuunganisha kwa sababu nafasi yake katika tungo hizo si nafasi ya kiunganishi ambatanishi katika lugha ya Kiswahili. Kuthibitisha hilo, tunaona kwamba neno "ama" likiondolewa bado tungo hizo zinabaki na maana ileile. Mifano ya (9a na b) inathibitisha hilo.

9. (a) Mtu aliyewahi kutiwa hatiani kwa ubadhirifu wa mali ya umma, [[katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano] au [Serikali ya Mapindizi ya Zanzibar]] hatakuwa na sifa ya kuteuliwa. (Katiba Inayopendekezwa, 2004:39)

   (b) Haitaruhusiwa kufungua shauri la madai kuhusu jambo lolote alilolitenda rais [[kabla] au [baada ya kushika madaraka]]. (Katiba Inayopendekezwa 2004:32)

Katika mifano ya (9a na b), neno "ama" limeondolewa bila kuathiri maana ya tungo hizo. Hii ina maana kuwa kuwepo kwa neno "ama" katika tungo hizo ni uziada kwa sababu halichangii maana katika tungo. Hivyo, ni wazi kuwa lugha ya Kiswahili haina viunganishi wiani yaani viunganishi viwili vinavyotumika kwa pamoja kama kiunganishi kimoja. Aidha, neno "ama" na "au" ni viunganishi ambatanishi viwili vinavyojitegemea, hivyo haviwezi kutumika kwa pamoja kuambatanisha vipashio viwili.

Hata hivyo, inaelekea utumizi wa viunganishi hivyo wiani umetokana na athari ya lugha ya Kiingereza kwa kuwa ina kiunganishi chenye muundo na maana sawa na "ama.....au" ambacho ni *either....or*. Kutokana na athari hiyo, kutumia viunganishi *ama...au* katika lugha ya Kiswahili ni uziada kwa sababu neno *ama* na *au* ni viunganishi huru; kila kimoja kinaweza kutumika peke yake ilihali katika lugha ya Kiingereza kiunganishi *either* 'ama' hakiwezi kutumika peke yake bila kiunganishi *or* 'au'. Hoja hii inajidhihirisha katika mifano ya (10a-d).

10. (a) Mashirika ya kimataifa [[kwa namna moja] **ama** [nyingine]] yamesaidia katika utekelezaji wa bajeti. (Wizara ya Fedha 2016/2017:6)
   (b) **International organizations have helped in one way **either** another to supplement the budget.* (Tafsiri yangu)
   (c) Mashirika ya kimataifa [[kwa namna moja] **au** [nyingine]] yamesaidia katika utekelezaji wa bajeti.
   (d) *International organizations have helped in one way **or** another to supplement the budget.* (Tafsiri yangu)

Mfano ya (10a) unaonesha kuwa neno "ama" katika lugha ya Kiswahili ni kiunganishi ambatanishi kinachojitegemea ilihali neno hilo katika lugha ya Kiingereza, yaani *either* haliwezi kusimama lenyewe kama kiunganishi ambatanishi kama mfano wa (10b) unavyoonesha. Hivyo, kwa kuwa neno hilo ni kiunganishi ambatanishi kinachojitegemea katika lugha ya Kiswahili, hakiwezi kutumika pamoja na kiunganishi kingine yaani "au" katika tungo moja kuambatanisha vipashio viwili. Hivyo, ni dhahiri kuwa tungo ambatani zenye viunganishi "ama...au" ni tungo ambazo zimeambatanishwa kwa kiunganishi "au" pekee na sio "ama...au". Tazama mfano wa (11) kwa uthibitisho zaidi.

11. (a) Sheria ambayo inaendelea kutumika **ama** [[bila mabadiliko] **au** [baada ya kubadilishwa] **au** [kurekebishwa]]... (Katiba Inayopendekezwa 2004:49)

    (b) Sheria ambayo inaendelea kutumika [[bila mabadiliko] au [baada ya kubadilishwa] au [kurekebishwa]]...

Katika mfano wa (11a), vipashio vilivyoambatanishwa ni zaidi ya viwili ambapo neno "ama" limetokea mara moja tu kabla ya kiambatanishwa cha kwanza ilhali kiunganishi "au" kimejirudia kati ya viambatanishwa vingine. Mfano wa (11b) unathibitisha kuwa kiunganishi "au" kinaweza kutumika peke ya bila kiunganishi "ama" na tungo ikabaki na maana ileile. Hivyo, ni wazi kuwa kiunganishi katika tungo (10a) ni "au" peke yake na si "ama......au".

*Viunganishi Ambatanishi Tenguzi*

Kundi jingine la viunganishi ambatanishi vilivyobainishwa katika utafiti huu ni viunganishi vinavyoashiria hali ya utenguzi au kinzani, ambavyo ni "lakini", "bali" na "ila". Data zinaonesha kuwa viunganishi hivi huunganisha tungo kama vile virai vitenzi, vishazi na sentensi. Viunganishi hivi huonesha hali ya kinyume na matarajio au utenguzi wa kile kilichotajwa awali kama inavyojidhihirisha katika mifano ya (12a-c).

12. (a) [[Najua kutumbua jipu kuna maumivu], **lakini** [bahati mbaya halina dawa nyingine]]. (Magufuli 20/11/2015:21)
    (b) [[Kile kichogo alichokuwa akikitazama K hakikuwa kichogo kamwe], **bali** [kitu chenye sura ya fuvu]]. (Mohamed, 2007:19)
    (c) [[Wafanyakazi zaidi ya 200 walilipwa mishahara], **ila** [ndege ni moja]]. (Magufuli 20/11/2015:6)

Viambatanishwa katika mifano ya (12a-c) ni sentensi na vishazi. Mifano hiyo inaonesha kwamba uambatanishaji kwa viunganishi linanuzi huhitaji pande mbili zinazokinzana. Kwa mfano, katika mfano wa (12a), ilitarajiwa kuwa, kwa kuwa "kutumbua jipu kuna maumivu" basi litumbuliwe lakini kinyume na matarajio lazima litumbuliwe kwa kuwa "bahati mbaya halina dawa nyingine". Vilevile, katika mfano wa (12b), kwa maelezo ya kishazi cha kwanza *K* alitarajia kuwa alichokuwa anakitazama ni kichogo lakini kinyume na matarajio inaelezwa kuwa "kile kichogo alichokuwa akikitazama K hakikuwa kichogo kamwe" kinyume chake, ni "kitu chenye sura ya fuvu". Halikadhalika, katika mfano wa (12c) inatarajiwa kuwa ikiwa "Wafanyakazi zaidi ya 200 walilipwa mishahara", basi ndege zitakuwa nyingi lakini kinyume na matarajio hayo, "ndege ni moja". Hivyo basi, viunganishi "lakini", "bali" na "ila" vinaashiria mahusiano ya hali ya utenguzi kati ya kiambatanishwa cha kwanza na cha pili.

Hata hivyo, kiunganishi "bali" hutofautiana kisemantiki na kiunganishi "lakini" kwa sababu uambatanishaji wake huashiria unyume kwa kupinga kile kilichoelezwa na kiambatanishwa cha kwanza kwamba si sahihi na kutoa majibu sahihi katika kiambatanishwa cha pili. Kutokana na hali hiyo, mara nyingi kiambatanishwa cha kwanza huwa na ukanushi kama mifano ya (13a-c) inavyodhihirisha.

13. (a) [[Mahali hapo hapakuwa na kichaka], bali [palikuwa na jangwa]]. (Abdulla, 1997:16)
    (b) [[Hawapiti hovyo hovyo njia hiyo], bali [huchagua nyakati za kupitia]]. (Abdulla, 1997:16)
    (c) [[Uhai wenyewe si wa binadamu], bali [uhai wa picha za binadamu]]. (Abdulla, 1997:19)

Mifano ya (13a-c) inaonesha kwamba kiambatanishwa cha kwanza kina ukanushi ambapo kiunganishi "bali" kinaashiria kwamba kiambatanishwa cha pili kinatoa maelezo yaliyosahihi juu ya kile kilichokanushwa katika kiambatanishwa cha kwanza. Kutokana na hali hiyo, kiunganishi "bali" huitwa kiunganishi rekebishi. Baadhi ya lugha kama Kiingereza hutumia kiunganishi *but* kurejelea "lakini" na "bali". Hata hivyo, kiunganishi *but* kinapotumika kama "lakini" huitwa kiunganishi cha kinyume na matarajio na kinapotumika kama "bali" huitwa

kiunganishi rekebishi (Vicente, 2010). Hivyo, wakati Kiingereza kinatumia umbo moja *but* kumaanisha "lakini" na "bali" Kiswahili hutumia maumbo mawili.

Pia, data za utafiti huu zinaonesha kuwa kiunganishi ambatanishi tenguzi "ila" kisemantiki nacho kina tofauti kidogo na viunganishi "lakini" na "bali". Kiunganishi hiki huashiria hali ya utenguzi kwa kuonesha kasoro juu ya kile kilichosemwa awali. Kiunganishi hiki hakipingi moja kwa moja taarifa iliyotolewa na kiambatanishwa cha kwanza, bali huonesha kasoro juu ya taarifa iliyoelezwa na kiambatanishwa cha awali. Kwa maneno mengine kiunganishi "ila" huonesha kwamba kilichoelezwa katika kiambatanishwa cha kwanza ni sahihi, isipokuwa taarifa hiyo ina upungufu au kasoro ambayo huelezwa na kiambatanishwa cha pili. Mifano ya (14a na b) inatoa ufafanuzi zaidi.

14. (a) [[Hawana miili tena] ila [wamebakia kama vivuli]]. ( Abdulla, 1997:20)
    (b) [[Waliendelea kitambo kikubwa vilevile kimyakimya], ila [Bwana Msa alikuwa akivuta kiko chake kwa nguvu]]. (Abdulla. 1997:34)

Mifano ya (14a na b) ina viambatanishwa viwili ambavyo ni vishazi. Viambatanishwa hivyo vimeambatishwa kwa kiunganishi 'ila'. Kiunganishi hicho kinaashiria kasoro au hitilafu juu ya taarifa ya kiambatanishwa cha kwanza. Kasoro au hitilafu hiyo huelezwa na kiambatanishwa cha pili. Kwa mfano, katika mfano wa (14a) taarifa inayoelezwa ni kwamba watu wanaozungumziwa "hawana miili tena" isipokuwa "wamebakia kama vivuli". Mfano wa (14b) unatoa taarifa kwamba "waliendelea na safari yao kwa kitambo kikubwa wakiwa kimya" isipokuwa "Bwana Msa alikuwa akivuta kiko chake kwa nguvu". Kutokana na hali hiyo, kiunganishi "ila" huashiria kwamba maelezo au taarifa iliyotolewa na kiambatanishwa cha kwanza ina kasoro ambayo hurekebishwa kwa kiambatanishwa cha pili.

*Kiunganishi Ambatanishi Kanushi*

Kiunganishi kanushi kilichobainishwa kwenye utafiti huu ni "wala". Kiunganishi hiki hufanya kazi katika mazingira ya ukanushi ambapo viambatanishwa vyote hukanushwa. Mifano ya (15a na b) inafafanua zaidi.

15. (a) Hapaoti [[miti] **wala** [majani]]. (Abdulla, 1997:16)
    (b) [[Hawakumuona]] **wala** [hawakupata habari timamu]]. (Abdulla, 1997:10)

Katika mifano hiyo ukanushi umewekwa mwanzoni mwa sentensi na kiunganishi kanushi "wala" kimewekwa kati ya viambatanishwa. Mathalani, katika mfano wa (15a) ukanushi uliopo kwenye kitenzi unaonesha kuwa mahali hapo "hapaoti miti" na kiunganishi "wala" kinaongezea kwamba pia "hapaoti majani". Hivyo, kati ya miti na majani, hakuna kinachoota mahali hapo. Vivyo hivyo, katika mfano wa (15b) kiunganishi "wala" kinaonesha kwamba, si tu "hawakumwona", bali "hawakupata habari timamu" pia. Tungo hiyo inaweza kufafanuliwa kuwa "hawakumuona" na "hawakupata taarifa yoyote". Vilevile, mfano wa (15a) unaweza kufafanuliwa kama "ukanushi A au B" (taz. mfano wa 16a) au kama "ukanushi A na ukanushi B" (taz. 16b) ambapo A ni kiambatanishwa cha kwanza na B ni kiambatanishwa cha pili.

16. (a) Hapaoti [[miti] **au** [majani]]. (Abdulla, 1997:16)
    (b) [[Hapaoti miti] **na** [hapaoti majani]].

Ingawa kiunganishi "au" katika mfano (16a) kinatoa fursa ya kuchagua kati ya "miti" na "majani", ukanushi uliotangulia mwanzoni mwa sentensi unazuia uchaguzi huo. Katika mfano wa (16b), kiambatanishwa cha kwanza kinaeleza kwamba mahali hapo "hapaoti miti" na kiunganishi ongezi "na" kimeongezea kwamba "hapaoti majani". Mapitio ya maandiko yanaonesha kuwa katika lugha nyingi kiunganishi kanushi huwa ni jozi wiani yaani maumbo mawili wiani.

Kwa mfano, Haspelmath (2004), anaeleza kuwa lugha za Ulaya na baadhi ya lugha zisizo za Ulaya kiunganishi kanushi huwa ni maumbo mawili wiani. Miongoni mwa lugha hizo ni lugha ya Kiingereza ambayo kiunganushi kanushi ni *neither...nor* "wala", Kijerumani *weder ...noch,* "wala", Kiitaliano *ne...ne* "wala". Hii ndiyo sababu Ashton (1947) katika orodha ya viunganishi ambatanishi vya Kiswahili, aliorodhesha kiunganishi chenye jozi wiani "wala...wala". Hata hivyo, data za utafiti huu zinaonesha kuwa Kiswahili hakina kiunganishi chenye jozi wiani bali kina umbo moja "wala".

*Viunganishi Ambatanishi vya Wakati*

Viunganishi ambatanishi vinavyoashiria uwakati vilichobainishwa katika utafiti huu ni "kisha" na "halafu". Viunganishi hivi huambatanisha matukio yanayofuatana kiwakati kama mifano namba (17a na b) inavyoonesha.

17. (a) Aliniamuru [[nimpe leseni], **kisha** [niegeshe gari langu pembeni]].
    (Mwananchi 30/4/2017:3)
    (b) [[Bwana Msa alitulia tu], **halafu** [alijizoazoa]], akajinyoosha mwili wake. (Abdulla, 1997:19)

Kiunganishi *kisha* katika mfano wa (17a) kinaonesha kuwa tukio la “kumpa leseni” lilitangulia kiwakati tukio la “kuegesha gari”. Hii ina maana kwamba tukio la kishazi cha kwanza linafuatana kiwakati na tukio la kishazi cha pili. Hivyo, kabla ya kuegesha gari, alitakiwa kutoa leseni kwanza. Vivyo hivyo, katika mfano wa (17b), tukio la tukio la “kujizoa” lilifuata baada ya tukio la “kutulia”. Aina za viunganishi ambatanishi katika lugha ya Kiswahili zimelezwa kwa msingi wa sarufi ya lugha ya Kiswahili bila kutumia modeli za lugha nyingine kama Nadharia Msingi wa Isimu inavyotaka. Aidha, maarifa ya kitaipolojia kutoka kwa tafiti tangulizi yamewezesha kuona upekee wa lugha ya Kiswahili katika kipengele hiki.

**Kiswahili ni Lugha ya Kiunganishi Kimoja**

Kwa kutumia Nadharia Msingi ya Isimu, maarifa ya kitaipolojia kuhusu aina za lugha katika utumizi wa viunganishi ambatanishi yanaonesha kuna aina mbili za lugha katika matumizi ya viunganishi ambatanishi dhahiri (Haspelmath, 2000). Aina hizo ni lugha za kiunganishi kimoja na lugha za viunganishi vingi. Lugha za kiunganishi kimoja ni zile zinazotumia kiunganishi ambatanishi kimoja kuambatanisha vipashio viwili kama mfano namba (18) unavyoonesha. Lugha za viunganishi vingi ni lugha zinazotumia viunganishi viwili au zaidi kuambatanisha vipashio viwili kama mfano namba 19 unavyoonesha.

18. (a) Hapaoti [[miti] **au** [majani]]. (Abdulla, 1997:16)
    (b) [[***àti*** *èmí*] [***àti*** *Kéhìndé*]]. (Haspelmath, 2004:10)
    *Na mimi na Kehinde*
    “Mimi na Kehinde”

Viunganishi ambatanishi katika mifano namba (18 na 19) vimeandikwa kwa wino uliokozwa. Mfano namba (18) unawasilisha tungo ambatani ya Kiswahili yenye kiunganishi ambatani kimoja ambacho kimewekwa katikati ya viambatanishwa. Mfano namba (19) unawasilisha tungo ambatani kutoka lugha ya Kiyoruba ambayo ina viunganishi ambatanishi viwili vilivyowekwa kabla ya kila kiambatanishwa.

Tukichunguza idadi ya vipashio vilivyoambatanishwa katika mifano hiyo miwili ni viwili ambavyo katika lugha ya Kiswahili vimeambatanishwa kwa kiunganishi kimoja, lakini katika lugha ya Kiyoruba vimeambatanishwa kwa viunganishi viwili. Hivyo, Kiswahili ni miongoni mwa lugha ya kiunganishi kimoja ambacho huwekwa kati ya viambatanishwa na Kiyoruba ni lugha ya viunganishi viwili ambavyo huwekwa kabla na baada ya kiambatanishwa cha kwanza.

Tafiti zinaonesha kwamba lugha za kiunganishi kimoja hutumia kiunganishi kimoja hata kama vipashio vinavyoambatanishwa ni vingi (Dik, 1968 na Oirsow, 1987). Tazama mfano namba (19) kwa ufafanuzi zaidi.

19. Tutahakikisha [[kila kijiji kinakuwa na zahanati], [kila kata inakuwa na kituo cha afya], [kila wilaya inakuwa na hospitali] **na** [kila mkoa unakuwa na hospitali ya rufaa]]. (Magufuli 20/11/2015:21)

Mfano namba (19) ni tungo ambatani yenye viambatanishwa vinne vilivyoko kwenye mabano. Vipashio hivyo vimeambatanishwa kwa kiunganishi kimoja kilichowekwa kati ya viambatanishwa viwili vya mwisho. Hii inathibitisha kile kinachoelezwa na baadhi ya wataalamu kama Dik (1968) na Oirsow (1987) kwamba hata katika uambatanishaji wa vipashio vingi kiunganishi huwa kimoja tu kwa lugha za kiunganishi kimoja.

Pia, Kiswahili ni lugha inayoweka kiunganishi ambatanishi kati ya viambatanishwa, tofauti na lugha nyingine ambazo kiunganishi kinaweza kuwa kabla ya kila kiambatanishwa, au baada ya kila kiambatanishwa, au mwishoni mwa viambatanishwa vyote (Taz. Drellishak 2005). Mfano namba (20a na b) unafafanua zaidi.

20. (a) Hatuna budi [[kuongeza mapato] **na** [kupunguza matumizi ya serikali]].
    (Magufuli 20/11/2015:21)
    (b) Tutahakikisha [[kila kijiji kinakuwa na zahanati], [kila kata inakuwa na kituo cha afya], [kila wilaya inakuwa na hospitali] **na** [kila mkoa unakuwa na hospitali ya rufaa]]. (Magufuli 20/11/2015:21)

Viambatanishwa katika mfano (20a) ni viwili na vimewekwa kwenye mabano. Tunaona kwamba kiunganishi kilichotumika kuviambatanisha ni kimoja ambacho kimewekwa kati ya viambatanishwa hivyo. Katika mfano wa (20b), viambatanishwa vinne lakini kiunganishi dhahiri kilichotumika kuviunganisha ni kimoja ambacho kimewekwa kati ya viambatanishwa viwili vya mwisho. Hii inaonesha kwamba Kiswahili ni lugha ya kiunganishi dhahiri kimoja na kiunganishi hicho huwekwa kati ya viambatanishwa ikiwa viambatanishwa hivyo ni viwili, na huwekwa kati ya viambatanishwa viwili vya mwisho ikiwa viambatanishwa ni zaidi ya viwili.

Hata hivyo, makala hii imebaini kuwa kuna mazingira machache sana ambayo kiunganishi huwa hakidondoshwi kinapoambatanisha viambatanishwa vingi bali huachwa dhahiri kati ya viambatanishwa vyote. Kwa mujibu wa Haspelmath (2000), hali hiyo hudhihirika katika lugha nyingi zinazoruhusu udondoshwaji wa kiunganishi ambatanishi katika tungo yenye viambatanishwa vingi. Mtaalamu huyo anaendelea kueleza kuwa kiunganishi kinapoachwa wazi kati ya viambatanishwa vyote huwa na dhima ya kuonesha msisitizo na ni mahususi au hutokea tu katika mazingira maalumu.

Makala hii imebaini kuwa kiunganishi kinapotumika kati ya kila kiambatanishwa huwa na dhima maalumu ya kimawasiliano kama vile kuonesha msisitizo na sio kuambatanisha vipashio kwa kuwa vipashio hivyo vinaweza kuambatanishwa bila kiunganishi dhahiri. Tazama mifano ya (21a na b), inavyoonesha.

21. (a) Alipokwisha [[kusafisha kila kitu] na [kufua] na [kukoga] na [kujirashia mafuta mazuri]]; alikuwa tayari kuondoka. (Mohamed, 2007:14)
    (b) Kasri hilo hukuziwa heba kwa mataa yanayoligandama shingoni huku [[yakimetameta] na [kung'aa] na [kupwitapwita] na [kukonyezakonyeza]]. (Mohamed, 2007:16)

Katika mifano ya (21a na b) kiunganishi 'na' hakikudondoshwa ingawa kimetumika kuambatanisha viambatanishwa vingi. Kiunganishi hicho kimerudiwa kati ya kila kiambatanishwa ili kuonesha msisitizo. Kwa mfano, kwa mujibu wa data, anayezungumziwa katika mfano wa (21a) ni waziri na kwa kawaida waziri kwa hadhi yake hategemewi kufanya shughuli zilizotajwa katika mfano huo. Kutokana na hali hiyo, kiunganishi 'na' kimewekwa kati ya kila kiambatanishwa ili kuonesha msisitizo wa yale aliyoyafanya waziri kwa sababu si kawaida waziri kufanya hayo. Hii ina maana kwamba, ingekuwa ni kawaida waziri kufanya hayo aliyoyafanya, kiunganishi kisingewekwa kati ya kila kiambatanishwa bali kingewekwa kati ya viambatanishwa, viwili vya mwisho.

Pia, katika mfano wa (21b), kiunganishi 'na' kimewekwa kati ya kila kiambatanishwa kwa ajili ya kuonesha msisitizo wa upekee wa mataa ya kasri. Hii ina maana kwamba mataa yanayozungumziwa katika mfano huo si ya kawaida; ni mataa yenye sifa nyingi zisizo za kawaida. Mwandishi anatumia kiunganishi 'na' kati ya kila kiambatanishwa ili kusisitiza sifa au upekee wa mataa hayo. Ufafanuzi wa data katika kipengele hiki yamethihirisha maarifa ya kitaipolojia na umahususi au upekee wa lugha ya Kiswahili kulingana na maarifa hayo. Hii imesaidia kubaini utofauti na ufanano wa lugha ya Kiswahili na lugha nyingine.

**Viunganishi Ambatanishi na Kategoria za Viambatanishwa**

Kwa kutumia msingi wa kidhima wa Nadharia ya Msingi ya Isimu, makala hii imebaini kuwa, katika lugha ya Kiswahili, viambatanishwa vinaweza kuwekwa katika makundi mawili kutokana na matumizi ya viunganishi ambatanishi. Kuna kundi la viambatanishwa vilivyobeba matukio tu, yaani virai vitenzi, vishazi na sentensi. Katika sehemu hii, kundi hili limeitwa vishazi kwa sababu katika mazingira mengi, ni vigumu kutofautisha virai vitenzi, vishazi na sentensi kwa kuwa huingiliana. Hoja hii inaungwa mkono na Haspelmath (2004:8) anayeeleza kwamba virai vitenzi, vishazi na sentensi huwekwa pamoja kwa sababu haijawa wazi ni kigezo gani kinaweza kutumika kuvitofautisha.

Kundi jingine ni viambatanishwa ambavyo havijabeba matukio kama vile aina zote za maneno isipokuwa vitenzi, na aina zote za virai isipokuwa virai vitenzi. Katika sehemu hii kundi hili limeitwa virai kwa sababu maneno yanaweza kuwa na hadhi ya virai pia. Makundi hayo mawili yametumika kwa sababu data zinaonesha kuwa kuna viunganishi ambatanishi vinavyoambatanisha viambatanishwa vilivyobeba matukio pekee na vingine huambatanisha makundi yote mawili. Jedwali namba 1 linaonesha viunganishi ambatanishi vya Kiswahii na kategoria za viambatanishwa zinazoweza kuunganishwa na kila kiunganishi.

**Jedwali Na. 1: Viunganishi Ambatanishi na Kategoria za Viambatanishwa**

| Viunganishi ambatanishi | Kategoria ya viambatanishwa | |
|---|---|---|
| | Virai | Vishazi |
| Na | √ | √ |
| Tena | √ | √ |

| | | |
|---|---|---|
| Pia | √ | √ |
| pamoja na | √ | √ |
| Au | √ | √ |
| Ama | √ | √ |
| Wala | √ | √ |
| Lakini | √ | √ |
| Ila | × | √ |
| Bali | × | √ |
| Halafu | × | √ |
| Kisha | × | √ |
| alama ya mkato wa kiimbo | × | √ |

**Chanzo:** Data za utafiti

Jedwali Namba 1 linaonesha kuwa kuna viunganishi ambavyo huambatanisha kategoria zote yaani virai na vishazi ilihali kuna vingine huambatanisha vishazi pekee.

Tafiti zinaonesha kuwa katika lugha nyingi duniani kiunganishi kichaguzi ndicho chenye uwezo wa kuambatanisha kategoria zote za viambatanishwa. Kwa kiasi kikubwa kiunganishi kiongezi na kiunganishi tenguzi huwa na maumbo tofauti ya kuambatanisha virai na vishazi (taz. Welmers, 1973, Abdoulaye, 2004 na Lefebvre, 2004). Hata hivyo, hali ni tofauti katika lugha ya Kiswahili. Data zinaonesha kuwa lugha ya Kiswahili haina maumbo mawili au zaidi ya kiunganishi 'na' au 'lakini'. Hivyo, kiunganishi 'na' hutumika kuambatanisha virai na vishazi katika lugha ya Kiswahili. Pia, kiunganishi kichaguzi 'au' na tenguzi 'lakini' navyo hutumika kuambatanisha viambatanishwa vyote virai na vishazi. Tazama mifano (22a na b), (23a na b) na (24) kwa ufafanuzi zaidi.

22. (a) Bwana yule alikuwa ameazimia [[shana] na [ubaya]].
    (b) Mimi [[nimewaahidi wananchi], na [nataka nirejee ahadi yangu kwao]].
23. (a) [[Vyama vya kitaaluma] au [wafanyakazi]] vimekuwa chachu ya ushindi katika chama cha siasa (Mtanzania 30/4/2017:3)
    (b) [[Mtu aliyekamatwa] au [aliyewekwa kizuizini]] ana haki ya kuelezwa sababu ya kukamatwa kwake. (Katiba Inayopendekezwa 2004:15)
24. [[Mimi nitaweza kuendelea kueleza vizuri zaidi], lakini [katika maelezo yangu nitatumia Kiswahili changu mwenyewe]]. (Abdulla 1997:63)

Viambatishwa vilivyoko kwenye mabano katika mfano namba (22a) ni virai nomino wakati katika mfano (22b) ni vishazi. Vipashio hivyo vimeambatanishwa kwa kiunganishi 'na'. Vivyohivyo, katika mfano (23a) kiunganishi 'au' kimeambatanisha virai nomino wakati katika (23b) kimeambatanisha vishazi. Vilevile, katika mfano namba (24) kiunganishi 'lakini' kimeambatanisha vishazi. Haya yanadhihirisha kile kinachoelezwa na Nadharia Msingi ya Isimu kwambani ni muhimu kuelewa masuala ya kiisimu kama vile miundo ya kiisimu kulingana na dhima zake katika lugha. Hivyo, katika kipengele hiki, elementi za kisarufi ambazo ni viunganishi ambatanishi zimedhihirisha namna zinavyotimiza lengo la mawasiliano.

**Viunganishi Ambatanishi na Idadi ya Viambatanishwa**

Makala hii imebaini kwamba Kiswahili kina viunganishi vinavyoambatanisha viambatanishwa viwili tu na vinavyoambatanishwa viambatanishwa zaidi ya viwili. Kwa mujibu wa Haspelmath (2004) lugha zote huruhusu uambatanishaji wa viambatishwa vingi (zaidi ya viwili) kwa kutumia viunganishi ongezi au vichaguzi. Hali hii inadhihirika pia katika lugha ya Kiswahili kama jedwali namba 2 linavyoonesha.

Hata hivyo, katika uambatanishaji wa viambatanishwa vingi kuna ruwaza mbili. Ruwaza ya kwanza ni lugha zinazoweka kiunganishi kila baada ya kiambatanishwa isipokuwa kiambatanishwa cha mwisho yaani *A u B u C u D…* ambapo 'ABCD' ni viambatanishwa na 'u' ni kiunganishi. Ruwaza ya pili ni kudondosha kiunganishi na kuacha kimoja tu baina ya viambatanishwa viwili vya mwisho. Makala hii imebaini kuwa Kiswahili hufuata ruwaza ya pili ya kudondosha viunganishi na kuacha kimoja tu baina ya viambatanishwa viwili vya mwisho. Hii ina maana kwamba baadhi ya viunganishi ambatanishi huweza kutumika kuunda tungo ambatani zenye urefu usio na kikomo kwa kuongeza idadi ya viambatanishwa na viunganishi ilihali viunganishi vingine hutumika kuunda tungo ambatini zenye viambatanishwa viwili pekee. Jedwali Na. 2 linaonesha idadi ya viambatanishwa vinavyoweza kuambatanishwa na kila aina ya kiungashi ambatanishi katika lugha ya Kiswahili.

**Jedwali Na. 2: Viunganishi Ambatanishi na Idadi ya Viambatanishwa**

| **Viunganishi** | **Idadi ya Viambatanishwa** | |
|---|---|---|
| | **Viambatanishwa Viwili** | **Viambatanishwa zaidi ya Viwili** |
| Na | √ | √ |
| Tena | √ | x |
| Pia | √ | x |
| pamoja na | √ | √ |
| Au | √ | √ |
| Ama | √ | x |
| Lakini | √ | x |
| Ila | √ | x |
| Bali | √ | x |
| Wala | √ | √ |
| Halafu | √ | x |
| Kisha | √ | x |
| alama ya mkato | √ | √ |

**Chanzo:** Data za utafiti

Jedwali Namba 2 linaonesha kuwa viunganishi ambatanishi hutofautiana kimatumizi kwani kuna vinavyoweza kuambatanisha vipashio zaidi ya viwili ilihali vingine huambatanisha vipashio viwili tu. Hali hii inaonesha kuwa lugha inaweza kuwa na viunganishi ambatanishi kadhaa ambavyo matumizi yake hayafanani. Katika lugha ya Kiswahili tumeona kuna viunganishi vinavyoambatanisha viambatanishwa viwili tu na kuna vinavyoambatanisha viambatanishwa zaidi ya viwili. Hii ina maana kwamba uambatanishaji wa viambatanishwa vingi katika lugha ya Kiswahili unakubalika lakini sio kila kiunganishi ambatanishi kinaweza kuambatanisha viambatanishwa vingi. Matumizi ya viunganishi ambatanishi kulingana na idadi ya viambatanishwa yanadhihirisha msingi wa dhima wa Nadharia Msingi ya Isimu kwamba ni muhimu kuelewa masuala ya kiisimu na namna yanavyotimiza lengo la mawasiliano.

**Hitimisho**

Makala hii imejadili uambatanishaji katika lugha ya Kiswahili. Mambo yaliyojadiliwa ni pamoja na aina ya uambatanishaji iliyopo katika lugha ya Kiswahili, aina za viunganishi ambatanishi katika lugha ya Kiswahili na matumizi ya viunganishi ambatanishi katika lugha ya Kiswahili kulingana na aina na idadi ya viambatanishwa. Mambo haya yamejadiliwa kwa misingi ya Nadharia Msingi ya Isimu. Pamoja na mambo mengine, imebainika kwamba Kiswahili kina uambatanishaji wa viunganishi dhahiri na uambatanishaji bila viunganishi dhahiri. Pia, imebainika kwamba Kiswahili ni lugha ya kiunganishi kimoja tu ambacho huwekwa kati ya viambatanishwa, yaani baada ya kiambatanishwa cha kwanza au kabla ya kiambatanishwa cha pili. Vilevile, imebainika kuwa Kiswahili hakina maumbo mawili ya kiunganishi "na" kwa ajili ya kuambatanisha virai kama ilivyo kwa lugha nyingi za Afrika (taz. Welmers 1973, Abdoulaye 2004, Lefebvre 2004). Aidha, imebainika kwamba Kiswahili hakina viunganishi wiani kama ilivyo kwa baadhi ya lugha za Ulaya. Hata kiunganishi cha ukanushi imebainika kwamba kina umbo moja tu ambalo ni "wala" na sio "wala … wala". Mwisho, makala imebaini kwamba viunganishi ambatanishi vya Kiswahili hutumika kwa namna tofauti kulingana na aina na idadi ya viambatanishwa. Vipo vinavyoambatanisha vishazi pekee na vinavyoambatanisha vishazi na virai. Pia, vipo vinavyoambatanisha viambatanishwa viwili tu na vinavyoambatanisha viambatanishwa vingi.

**Mgongano wa maslahi**
Mwandishi anakiri kwamba hakuna mgongano wa kimaslahi kuhusiana na uandishi na uchapishaji wa makala hii.

**Udhamini**
Mwandishi anakiri kwamba hakupata udhamini wowote wa kifedha kutoka kwenye taasisi yoyote kwa ajili ya utafiti na uandishi wa makala hii.

**Marejeleo**

Abdoulaye, M. L. (2004). Comitative, Coordinating, and Inclusory Constructions in Hausa. Katika M. Haspelmath (Mh.). *Coordinating Constructions*. Amsterdam: Benjamins, 165-193.

Abdulla, M. S. (1997). *Mzimu wa Watu wa Kale*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Ashton, E. O. (1947). *Swahili Grammar.* London: Longmans Group Limited.

Camacho, J. (2003). *The Syntax of Coordination*. Dordrecht: Kluwer Academic Publishers.

Baker, C. L. (1978). *Introduction to Generative-transformational Syntax*. New Jersey: Prentice-Hall.

Dik, S. C. (1968). *Coordination: Its Implications for the Theory of General Linguistics*. Amsterdam: North-Holland Publishing Company.

Drellishak, S. (2005). *A Survey of Coordination Strategies in the World Languages*. Washington: Washington University Press.

Dryer, M. (2001). What is Basic Linguistic Theory? Katika Mathew Dryer's Homepage. Department of Linguistics, University at Buffalo.

Dixon, R. M. W. (2012). Basic Linguistic Theory Volume 3: Further Grammatical Topics (Juzuu. 3). Oxford. Oxford University Press.

Dixon, R. M. W.(2010). Basic Linguistic Theory Juz. 1: Methodology. Oxford. Oxford University Press.

Dzameshie, A. K. (1999). Structure of Coordination in Ewe, katika *Journal of West African Languages* XXV2.1, 35-41.

Haspelmath, M. (2007). Coordination. Katika T. Shopen (Mh.). *Language Typology and Syntactic Description*. Cambridge: Cambridge University Press, 1-51.

Haspelmath, M. (2004). *Coordinating Constructions*. Amsterdam: John Benjamins.

Haspelmath, M. (2000). Coordination. Katika T. Shopen (Mh.). *Language Typology and Linguistic Description (Toleo la 2).* Cambridge: Cambridge University Press.

Kombe, L. E. (2019). Uchambuzi wa Sintaksia ya Uambatanishaji katika Lugha ya Kiswahili, Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Dar es Salaam. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Lefebvre C. (2004). Coordinating Constructions in Fongbe with Reference to Haitian Creole. Katika M. Haspelmath (Mh.). *Coordinating Constructions*. Amstadam: Benjamins, 123-164.

Magufuli, J. P. J. (2015). Hotuba ya Ufunguzi wa Bunge Jipya la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Dodoma: Ikulu.

Matthews, P. H. (2007). *Concise Dictionary of Linguistics*. New York: Oxford University Press.

Mithun, M. (1988). The Grammaticalization of Coordination. Katika J. Kaiman na S. A. Thompson (Wah.). *Clause Combining in Grammar and Discourse*. Amsterdam: Benjamins, 331-359.

Oirsouw, R. (1987). *The Syntax of Coordination*. London: Croom Helm.

Payne, T. & Weber, D. (2007). *Perspectives on Grammar Writing.* Amsterdam: John Benjamins.

Ramat, A. & Mauri, C. (2011). *The Grammaticalization of Interclausal Connectives*. Oxford: Oxford University Press.

Sanders, G. A. (1977). A functional Typology of Elliptical Coordination. Katika F. R. Eckman (Mh.). *Current Themes in Linguistics: Bilingualism, Experimental Linguistics, and Language Typologies*. Washington, DC: Hemisphere, 241-70.

Schachter, P. (1977). Constraints on Coordination. Katika Jarida la *Language*, 53(1): 86-103.

Stassen, L. (2000). AND-languages and WITH-languages. Katika Jarida la *Linguistic Typology*, 4(1): 1-55.

Vicente, L. (2010). On the Syntax of Adversative Coordination. Katika Natural Language & Linguistic Theory, 381-415.

Wälchli, B. (2003). *Co-compounds and Natural coordination*. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Stockholm.

Welmers, E. (1973). *African Languages Structures*. London: University of Calfonia Press.

Zhang, N. N. (2006). On the Configuration Issue of Coordination, katika Jarida la *Language and Linguistics*, 7(1): 175-223.

Zhang, N. N. (2009). *Coordination in Syntax*. Taipei: Chuo Kikuu cha Taifa cha Chung–Chung.

**Wasifu wa Mwandishi**

**Dr. Luinasia Elikunda Kombe** ni Mhadhiri Mwandamizi wa Kiswahili isimu katika Idara ya Lugha na Fasihi, Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam kuanzia mwaka 2010. Kwa miaka 15 amekuwa akifundisha kozi mbalimbali za Kiswahili isimu kwa wanafunzi wa Shahada ya kwanza, Umahiri na hata Uzamivu. Hata hivyo, eneo lake la utaalamu ni pamoja na sintaksia ya Kiswahili na Lugha nyingine za kiafrika, ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya kigeni/ya pili.